Kuokolewa Kwa Nuhu Na Nyumba Yake
(The Saving of Noah and His House)

Na

John Kombo Nandwa

Kuokolewa Kwa Nuhu Na Nyumba Yake

Na

John Kombo Nandwa

Octoba 9, 2014

Kuokolewa Kwa Nuhu Na Nyumba Yake

Biblia inasema, "*Kwa imani Nuhu akisha kuonywa na Mungu katika habari ya mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akahukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.*" (Heb. 11:7).

Uovu uliokuwepo kipindi cha Nuhu ulikuwa mkubwa kiasi kwamba Nuhu asingeweza kuokoa yeyote isipokuwa watu wa nyumbani kwake. Hataivyo, hawezi kuitwa kuwa alishindwa. Watu wakuu kama Daudi na Samweli hawakufanikiwa sana katika jitihada za kuwaokowa watoto wao, na kwaiyo wanakwenda nyuma sana ya Nuhu. Si ingekuwa vuzuri kama kila Mkristo leo angeweza kuokoa watoto wake wote! Hakika Nuhu alitengeza mji wenye mafanikio.

Leo hi kwa sababu ya madhehebu mengi yanayoanzishwa na wanadamu, ni kawaida kuona familia zinagawanyika, kuhusu ni kanisa lipi au dhehebu lipi baba au mama anapaswa kuhudhuria. Watoto huchanganyikiwa ama kumfuata baba au mama. Yoshua aliwaambia wana wa Israeli "...mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana." (Yosh. 24:15). Katika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo, baadhi ya sifa zilizoorodheshwa ni "*mwenye kuisimamia nyumba yake vyema ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?*" (1 Tim.3:4-5).

Tukirudi katika Mwanzo 6:5 tunasoma, "*BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya sikuzote.*" Katika msitari wa 6 Biblia inasema, "*BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo.*" Bwana aakaamua kumuangamiza mwanadamu aliyemuumba, lakini Nuhu alipata neema machoni pa Mungu (Mwa. 6:7-8). Alipataje neema kama hiyo? Biblia inasema, Nuhu alikuwa mwenye hhaki, mkamilifu na aalitembea pamoja na Mungu.

Bado Mungu anawaangalia wanadamu waaminifu ili kuitimiza kazi yake duniani leo. Je wewe pia ni mmoja kati yaa wale watu waaminifu ambao Mungu huwatafuta?

Mpango wa Mungu na kazi yake ilikuwa ni kuangamiza mwanadaamu, wanyama na vitambaavyo na ndege wa angani. Mwanzoni Mungu aalitabiri katika Mwa. 3:15 aliposema, "*nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, nawe atakugonga kichwa naye atakugonga kisigino.*" Hivyo basi, ilikuwa ni muhimu uzao wa mwanamke utunzwe kupitia mtu mwaminifu. Mtu huyo angepaswa kuteuliwa kwa makini; Nuhu alikuwa na sifa ya kutenda kazi njema.

Nuhu alipewa mpango wa Mungu. Aliambiwa kutengeneza, "*Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. Hivi ndivyo utaakavyoifanya, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na ya tatu.*" (Mwa. 6:14-16). Biblia inasema, "*kwa imani Nuhu akisha kuonywa na Mungu kuhusu mambo yasiyoonekana bado, alijawa hofu, akatengeneza safina ili kuiokoa nyumba yake…*" (Heb. 11:7). Nuhu alitii agizo pekee la Mungu na maelekezo kujenga safina. Kama asingetii hasingewaokoa familia na nyumba yake. Haki ya Nuhu inamweka katika daraja la peke yake kilaa ukifikiria mioyo ya maelefu ya wanadamu ilikuwa miovu kila wakati.

Haikujalisha wengine walifanya nini, Nuhu alidhaamiria kufanya kile alichokisema Mungu, na alitenda – kila kitu. Katika mazingira yako na yangu tunaofanya kazzi katika kanisa la Kristo kuna madhehebu; wanafanya mambo ambayo sisi hatufanyi. Kama Nuhu, kwetu ni kutii na kufanya yale ambayo Biblia inasema. Tunapaswa kunena pale ambapo Biblia inanena na kunyamaza pale ambapo Biblia imenyamaza. Mungu amenena na tunapaswa kusikiliza na kuyafanya yale aliyoyaagiza. (Luka 6:46; Yoh. 12:48).

Mwisho, wale ambao hawakuwa ndani ya safina wasingeweza kuikimbia gharika. Hakika watu waliokuwa kwenye tope wasingeweza kukimbilia usalama wao, lakini maji yalikuwa yakiongezeka, yakipanda, na kupanda – hadi dunia yote ikamezwa na maji bila kuwa na tumaini na kila sauti iliyopiga kelele ilinyamazishwa. Maji yaliwasogeza waovu; lakini wana watiifu wa Mungu walikuwa salama. Waliendesha wakavuka gharika kwa sababu Mungu alikuwa naodha wa mashua yao na rubani wa wokovu wao.

Ukisoma mwanzo sura ya 7, mtu anaweza kuona kwamba uharibifu wa mwanadamu mwenye dhambi wakati wa Nuhu ulikamilika; ndivyo itakavyokuwa mwisho wa dunia wakati Mwana wa Mungu atakapokuja. Petro anasema, "*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika ssiku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya aasili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kaazi zilizomo ndaani yake zitateketea.*" (2 Pet. 3:10).

Ni nini "safina salama" ya Mungu leo?

Biblia inasema, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote kaatika vyote.*" (Efe. 1:22-23). Nuhu alipewa na mpango na Mungu wa kujenga safina ambao uliokoa familia ya watu nane. Yesu Kristo alikuja duniani kuijenga kanisa lake. Watu wote wa mataifa yote ya dunia wanaweza kuokolewa kwa kanisa ambalo Yesu Kristo alijenga. Mtume Paulo aliandika, "*Ili sasa kwa njia ya kanisa hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu war oho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu.*" (Efe. 3:10-11).

John Kombo

Nakuru Kenya